

UHUVU

## uvamizi wa mito na mabonde

mamba  
mabonde\*Ulega ataja mbinu\*  
kuepuka migogoro  
wakulima, wafugaji

Na MWANDISHI WETU, Kilwa

mikoa mbalimbali nanchi waheshimu uachana na uvamizi de.

ya awamu ya sita ya mazingira kuwa yo kila Mtanzania ilinzi wa mazingira wa kuwa serikali tubwa kutengeneza oharibiwa.

kikosi kazi hicho, Jeshi la Polisi, hicho kimefanikiwa iari za kukaa jirani walinzi wa watu anga.

umuhimu wa elimu ili wawe na ili serikali ijpange uriko yakija wawe nyumba nyingi kana na vitendo wanaovamia mito

VIONGOZI wa serikali kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, kata na wilaya wametakiwa kuhakikisha wanaunda kamati za maridhiano ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji.

Imeelezwa migogoro hiyo imekuwa ikijitokeza katika baadhi ya maeneo na kuleta madhara kwa jamii.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa agizo hilo juzi katika ziara aliyofanya Kijiji cha Nakiu, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, baada ya kupokea kero zilizohusu migogoro mingi iliyoanza kujitokeza wilayani humo inayowahusisha wakulima na wafugaji.

Katika mkutano huo, wananchi wa Kijiji hicho walililalamikia Jeshi la Polisi kutochukua hatua za haraka wanapopelekewa taarifa za wafugaji wanaolisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Wakulima hao walidai wafugaji wanaofanya vitendo hivyo, wengi ni wahamiaji katika maeneo hayo, hivyo wamekuwa wakisababisha matatizo makubwa yakiwemo kuharibiwa mazao yao.

Kutokana na malalamiko yaliyotolewa na sehemu kubwa ya wakulima hao, Waziri Ulega alitoa maelekezo kwa watendaji wa serikali kuanzia ngazi za chini kuanzisha



**Jeshi la Polisi Wilayani humo lihakikishe linatenda haki kwa kila mtu na kwa usawa ili kuondoa lawama zinazowakabili**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi  
Abdallah Ulega.

kamati za usuluhishi zishughulikie migogoro hiyo mapema kabla hajakuwa mikubwa na kuleta madhara.

"Jeshi la Polisi Wilayani humo lihakikishe linatenda haki kwa kila mtu na kwa usawa ili kuondoa lawama zinazowakabili za kuonekana wanawapendelea wafugaji kuliko wakulima," alisema Ulega.

Aidha, aliwaekeza watendaji wa wilayani humo kuwa katika kamati hizo watakazozuunda waandae mpango mzuri wa kuweka njia kwa ajili ya kupitishia mifugo ili isiwe inapita katika mashamba ya wakulima.

Waziri Ulega alitumia ziara hiyo pia kukemea vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vinavyofanywa na wakulima na wafugaji, akisema kuwa kufanya hivyo ni kosa na ni miongoni mwa vitendo vinavyochangia uvunjifu wa amani.

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa katika kuhakikisha maelekezo hayo ya Naibu Waziri yanafanywa kazi kwa haraka, aliwaagiza watendaji wake kuhakikisha kamati hizo zinaundwa ndani ya wiki moja.

Kuhusu suala la kuweka njia za mifugo, Zainab alitoa mwezi mmoja kwa wataalamu wa mifugo kwa kushirikiana na wafugaji na wakulima kuhakikisha njia hizo zinawekwa ili kupunguza usumbufu wa mifugo katika mashamba ya wakulima.

Aliwataka wafugaji kuchimba mabwawa ya maji kwa mifugo yao hatua ambayo itasaidia kupunguza migogoro ya mara kwa mara na wakulima.



s Salaam,

a leo

washtakiwa ta yakiwemo sa ya ugaidi, va kutumika na kufadhili

O

ta  
thibitisha  
no.



**HABARI KITAIFA**

# Kamati kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji

Na Mbaraka Kambona, KILWA

**N**AIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka viongozi wa serikali kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, kata na wilaya kuunda kamati za maridhiano kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikijitokeza katika baadhi ya maeneo na kuleta madhara kwa jamii.

Ulega alitoa agizo hilo kwenye ziara aliyoifanya Kijiji cha Nakiu, wilayani Kilwa, mkoani Lindi Septemba 13, 2021 baada ya kupokea kero zilizohusu migogoro mingi iliyoanza kujitokeza katika wilaya hiyo inayowahusisha wakulima na wafugaji.

Katika mkutano huo wananchi wa kijiji hicho walililalamikia Jeshi

la Polisi kutochukua hatua za haraka wanapopelekewa taarifa za wafugaji wanaolisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Walisema wafugaji wanaofanya vitendo hivyo wengi ni wahamiaji katika maeneo hayo na wanasababisha matatizo makubwa ikiwamo kuharibiwa kwa mazao yao na wanaotaka kulinda mazao yao wanaishia kupata kipigo.

Kufuatia malalamiko hayo, Waziri Ulega alitoa maelekezo kwa watendaji wa serikali kuanzia ngazi za chini kuanzisha kamati za usuluhishi ili ziwe zinashughulika na migogoro hiyo mapema kabla haijakuwa mikubwa na kuleta madhara.

Aliongeza pia kwa kulitaka Jeshi la Polisi wilayani humo kuhakikisha wanatenda haki kwa kila mtu

na kwa usawa ili kuondoa lawama zinazowakabili za kuonekana wanawapendelea wafugaji kuliko wakulima.

Vilevile, aliwaelekeza watendaji wilayani humo kuwa katika kamati watakazozuunda waandae mpan-go mzuri wa kuweka njia kwa ajili ya kupitishia mifugo ili isiwe inapita katika mashamba ya wakulima.

Waziri Ulega pia kukemea vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vinavyofanywa na wakulima pamoja na wafugaji akisema kuwa kufanya hivyo ni kosa na ni miongoni mwa vitendo vinavyochangia uvunjifu wa amani.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa, katika kuhakikisha maelekezo hayo ya Naibu Waziri yanafanyiwa kazi kwa haraka aliwaagiza watend-

aji wake kuhakikisha kamati hizo zinaundwa ndani ya wiki moja.

Kuhusu suala la kuweka njia za mifugo, Kawawa alitoa mwezi mmoja kwa wataalamu wa mifugo kwa kushirikiana na wafugaji na wakulima kuhakikisha njia hizo zinawekwa ili kupunguza usumbufu wa mifugo katika mashamba ya wakulima.

Mkuu wa Wilaya pia aliwataka wafugaji kuchimba mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo na kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza migogoro ya mara kwa mara na wakulima.

Kabla ya ziara hiyo ya Waziri Ulega wilayani humo, siku chache zilizopita wafugaji waliuawa kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji katika Kijiji cha Nanjilnji.



for the first quarter in 2020

Saha, expressing satisfaction with census preparations so far,

participate in the national census as it will help the government to

premises the night before are counted," he added.

Sept 15, 2021

THE GUARDIAN Page 2



Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega addresses residents of Nanjilnji village in Kilwa District yesterday, chiefly on disputes pitting herders against other villagers. Photo: Guardian Correspondent



cuses", said Prof Mbatawa.  
Dodoma Regional  
Commissioner, Antony  
Mtaka also thanked the  
government for such suc-

complete in 2023, and the  
airport will be able to serve  
1.5 million passengers a  
year.

DAILY NEWS Page 4 SEPT 15

# \* Minister: Form committees to mediate farmer-pastoralist disputes \*

DEPUTY Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega, has told local government authorities to form arbitration teams to resolve conflicts between pastoralists and farmers.

The minister's call comes in the wake of emerging regular disputes between the two groups, causing serious effects in communities, including killings.

Mr Ulega issued the order

during a visit to Nakiu Village in Kilwa District, Lindi Region on Monday this week after receiving complaints over reported several conflicts in the district involving farmers and pastoralists.

At the meeting, villagers condemned the Police Force in the District for not taking immediate action to stop the situation even after getting information.

The villagers informed the

minister that major cause of the conflicts was pastoralists grazing their cattle on farms.

Many pastoralists in the region are migrants and that they have been grazing their cattle on farms causing destruction of crops, something which irritate farmers.

Following the complaints made by several farmers, the deputy minister instructed government officials from the grassroots to set up arbitration

committees so that they can deal with the disputes at early stage before they become serious and more harmful.

He called on the Police Force in the district to ensure that they do justice to everyone in order to avoid blames that they favor pastoralists more than farmers.

He also advised the district officials to come up with a good plan for earmarking pathways for livestock so that

they do not cross farms.

Kilwa District Commissioner, Zainab Kawawa, instructed her executives to ensure that the committees are formed within a week in implementing the directives.

Over cattle passageway, Ms Kawawa issued one-month ultimatum to veterinarians in collaboration with pastoralists and farmers to ensure that such routes are put in place to address a prob-

lem of livestock entering the farms.

In addition, the District Commissioner also urged pastoralists to dig water ponds for their livestock as another measure to avoid clashes with farmers.

Prior to Minister Ulega's visit to the District, a few days ago some pastoralists were killed as a result of similar conflicts at Nanjilinjji Village.

ls for more

## RC Kagaiyai urges SIDO to be creative